Mwongozo Mfupi

kwa waalimu & wakufunzi wa watu wenye albinism

UNDER THE SAME SUN

© June 2010 Under The Same Sun

Toleo La Kwanza
ISBN 978-9987-9611-2-2

Mwongozo Mfupi

Kwa Waalimu & Wakufunzi Wa Watu Wenye Ulemavu Wa Ngozi.

Yaliyomo.

Kwako mwalimu---------- 1

Msaada wa kuona---------- 2

Ulinzi wa ngozi---------- 5

Wawezeshe kujifunza---------- 5

Wajengee heshima---------- 6

www.underthesamesun.com

Mpendwa Mwalimu na Mkufunzi,

Wewe ni wa muhimu!

Waalimu na Wakufunzi wana majukumu ya muhimu sana katika maisha ya wanafunzi wenye albinism.

Licha ya familia yake ya karibu, walimu na wakufunzi wanabeba jukumu la kumsaidia mwanafunzi mwenye albinism kukua, kujifunza, na hatimaye kugundua uwezo wake katika maisha.

Mwalimu au mkufunzi unaposoma maelezo haya na kuanza kutekeleza MWONGOZO huu MFUPI kwa vitendo utasaidia katika kuyabadilisha maisha ya wanafunzi wenye albinism.

Sisi wafanyakazi wa UNDER THE SAME SUN (UTSS) tunaahidi kusaidia juhudi zenu katika kutekeleza Hatua zifuatazo kwa kiwango cha juu cha uwezo wetu. Tafadhali usisite kuwasiliana nasi unapohitaji msaada kuhusiana na hili.

Wako mwaminifu,

Timu ya Under The Same Sun

MSAADA WA KUONA

1. Wasaidie wanafunzi wako wenye ulemavu wa ngozi kuona ubaoni na kwenye vitu vingine vya kusomea.

HATUA:

- Kuza maandishi yako ubaoni.
- Kama inawezekana tumia ubao mweusi tu

- Ubao wa kijani na mweupe unaleta ugumu wa kuona kwa wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi, kama hakuna kabisa ubao mweusi tafadhali ongea na wafanyakazi wetu kuhusu kupata ubao wa haraka.

- Acha ubao ukiwa “mweusi”

- Hii ni muhimu ili kule kuandikiwa kwa chaki nyeupe kukuze uwezo wake wa kusoma.

• Inapokulazimu kutumia ubao wa kijani au mweupe tafadhali acha ubao wa kijani katika ukijani wake na tumia chaki nyeupe tu.

• Pia acha ubao mweupe katika weupe wake ukiwa unatumia kalamu nyeusi tu.

• Panga upya darasa – Waalimu na wakufunzi ni lazima wafanye juhudi ya ziada kupanga upya darasa ili wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi wapangwe mbele ya darasa na kupewa nafasi karibu na ubao kama inavyohitajika. Pia wawekwe katikati ya ubao maana kwa kawaida mbao zetu ni ndefu hivyo akiwekwa upande wa kulia au kushoto bado itampa shida kuona, na zaidi Mwalimu, kama inawezekana tumia upande wa katikati ya ubao tu ili kuwarahisishia zaidi kuona

• Huu upangaji upya wa darasa ni lazima ufanyike ili mwanafunzi mwenye ulemavu wa ngozi asitumie nguvu sana katika mwanga wa jua kuona ubaoni.

• Toa nakala ya mafundisho yako. Kama imeshindikana kupanga upya darasa Waalimu na wakufunzi wanatakiwa kujiandaa kutoa nakala za mafundisho yao na kumpatia kila mwenye ulemavu wa ngozi katika madarasa yao.

• Kutoa nakala kutoka kwenye daftari la mwanafunzi mwenye uwezo zaidi sio wazo zuri sana japo inakubalika.

• Msaada wa kutoa nakala unapatikana hapa UNDER THE

SAME SUN bila gharama yoyote.

Waruhusu kutumia teknolojia: Wanafunzi wako wenye ulemavu wa ngozi wanaweza wakahitaji kutumia vifaa vidogo vya mkononi kama vile vifaa vya kukuza maandishi, hii in lazima iruhusiwe maana wanalenga kukuza uwezo wao wa kuona.

2. Wasaidie wanafunzi wako wenye ulemavu wa ngozi kusoma maandishi yaliyochapishwa

HATUA:

• Kuza mitihani na vijitabu vingine vya kujisomea: maswali ya mitihani notisi za Waalimu na vitu vingine vyovyote vya kujisomea vilivyotolewa nakala au kuchapishwa ni lazina viwe vinaeleweka na vyenye maandishi makubwa ya kutosha.

• Tafadhali shirikiana na wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi, au mfanyakazi wa UNDER THE SAME SUN kujua ukubwa wa maandishi unaofaa kwa wanafunzi hao.

• Msaada wa kutoa nakala unapatikana UNDER THE SAME SUN bila gharama yoyote.

• Muda zaidi wa kufanya mtihani: Tunashauri kwamba muda wa ziada ni lazima utolewe wa kuandika mitihani kwa wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi. (Inashauriwa, muda wa kawaida wa kufanya mtihani ongeza nusu ya mda huo) Hii ni muhimu hasa wakati maswali ya mitihani yanapokua na maandishi madogo na kama mitihani ilishatumika.

- Kama wanafunzi hawa watapatiwa muda zaidi, inashauriwa kuwa wawekwe sehemu nyingine mbali na wenzao ili suala la muda liweze kusimamiwa sawasawa.

ULINZI WA NGOZI

Mlinde na jua mwanafunzi wako mwenye ulemavu wa ngozi.

HATUA

- Loshen ya kuzuia mionzi ya jua - Hakikisha kua mwanafunzi wako mwenye ulemavu wa ngozi anatumia mafuta yanayolinda ngozi yake kila siku. Mafuta haya yanaweza kupatikana katika ofisi ya UNDER THE SAME SUN.
- Mavazi – Washauri wanafunzi kuvaa sketi ndefu,mashati ya mikono mirefu,suruali na kofia ambazo zinawakinga na jua hasa wanapokua nje ya darasa.
- Miwani ya jua – Waruhusu wanafunzi kuvaa miwani ya jua wanapokua darasani au nje ya darasa kama inavyohitajika.
- Shughuli/ kazi za nje ya darasa – Tafadhali wasamehe watu wenye ulemavu wa ngozi wasifanye kazi za nje ya darasa labda kama kazi hizo zinaweza kuhamishiwa katika sehemu yenye kivuli.

WAWEZESHE KUJIFUNZA

Muongoze mwanafunzi wako mwenye ulemavu wa ngozi katika kujifunza.

HATUA

- Ufuatiliaji endelevu: Mara kwa mara waulize wanafunzi wako wenye ulemavu wa ngozi kama wanaendelea vizuri na kama wanaelewa. Waulize kama kuna kitu chochote cha kufanya ili kuwasaidia. Ongea na mmoja mmoja ili aibu isije ikawa kikwazo cha wewe kugundua ukweli.
- Usaidizi kutoka kwa wanafunzi wenzao: Katika masomo ya kila siku na katika vipindi vya ziada. Waalimu wanaweza kuona kuwa inasaidia sana kama mwanafunzi mwenye uwezo mkubwa darasani kila mmoja akapatiwa mlemavu wa ngozi ili watu hawa waweze kupata msaada kutoka kwa wenzao.
- Upendo : Mwalimu usione kama ni mzigo, kero au taabu kuwa na wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi darasani kwako,tafadhali wapende, wajali na pia chukuliana nao katika udhaifu wowote, uwezo mdogo wa kuona unaweza kusababisha washindwe kumaliza kazi kwa wakati, lakini usichoke, usiwafokee wala kuwaharakisha wape muda wasaidie huku ukiwatia moyo, sehemu kubwa ya mafanikio yao inategemea jinsi wewe mwalimu unavyowalea, wafanye wajione kuwa ni sehemu ya watoto wapendwao. Na hii itawafanya wawe na ujaasiri na wazidi kuongeza juhudi binafsi katika masomo yao

WAJENGEE HESHIMA.

Waongoze wanafunzi wako kwa mifano katika kuwafundisha wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi kwa uangalifu na heshima kama wafanyiwavyo wengine.

HATUA:

Saidia kumaliza uongo ufuatao: na usaidie kukuza uelewa wa kweli zifuatazo

Ukweli wa mwisho kwa waalimu na wakufunzi:

Watu wenye ulemavu wa ngozi ni binadamu kama wewe. Wanahitaji kutunzwa, kuangaliwa, na kulindwa ili wasiathiriwe na jua. Uwezo wao wa kuona ni mdogo na wanahitaji msaada wako katika kupambana na changamoto hizi wawapo darasani. Kwa msaada wako wanaweza kuwa wanafunzi wenye mafanikio na kutengeneza mchango mzuri ujao kwa jamii ya Tanzania.

UONGO: Mikosi, ugonjwa, balaa au kifo vyaweza kusababishwa na wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi.

UKWELI: kushirikiana nao hakutasababisha mikosi, magonjwa, balaa wala kifo bali itajenga uangalifu unyenyekevu na heshima ya utu.

UONGO: Mtu anaweza kupata ulemavu wa ngozi kama ugonjwa. UKWELI: huwezi kupata ulemavu wa ngozi kwa kua ni hali ya urithi iliyotoka kwa wazazi wote wawili kwenda kwa mototo, NA NI KWA NJIA YA UZAZI.

UONGO: Mtu anaweza kutumia viungo vya mtu mwenye ulemavu wa ngozi ili apone, atajirike, au afanikiwe.

UKWELI: Hakuna mtu atakayeweza kupata mafanikio, kutajirika,au kupona kwa kutumia viungo vya mtu mwenye ulemavu wa ngozi.

UONGO: Watu wenye ulemavu wa ngozi ni laana au ni mizimu.

UKWELI: Watu wenye ulemavu wa ngozi sio laana wala si mizimu. Ni wanadamu wenye aina Fulani ya urithi ambao wanastahili haki sawa kama ambavyo watanzania wengine wanapata Tafadhali waongoze watoto kuacha kutumia neno “Zeru-Zeru”.

Neno “Ulemavu wa Ngozi” linakubalika kwani linajaribu kukuza uelewa na heshima.

ASANTE KWA KUCHUKUA HATUA HIZI.

Kwa msaada na maelezo zaidi

WASILIANA NA UTSS TANZANIA
P. O Box 32837 DSM.
Tel: +255222780224,
Fax: +255222780224,
Email: info@utsstz.com

© June 2010 Under The Same Sun
Toleo La Kwanza
ISBN 978-9987-9611-2-2